

**draft report**  
**MATOKEO YA UCHAMBUZI WA UWAJIBIKAJI JAMII (SAM)**

**2010/11**

**WILAYA YA UKEREWE**



**November, 2012**

## Yaliyomo

Vifupisho .....	i <b>Error! Bookmark not defined.</b>
Shukrani.....	ii <b>Error! Bookmark not defined.</b>
Dibaji .....	iii <b>Error! Bookmark not defined.</b>
SEHEMU YA KWANZA .....	1 <b>Error! Bookmark not defined.</b>
1.0 Utangulizi .....	1 <b>Error! Bookmark not defined.</b>
1.1 Makubaliano ya Forum Syd na Policy Forum.....	1
SEHEMU YA PILI .....	2
2.0. Uchambuzi wa taarifa na matokeo .....	
.2 <b>Error! Bookmark not defined.</b>	
2.1 Mgawanyo wa rasilimali na Mpango Mkakati.....	2 <b>Error! Bookmark not defined.</b>
2.2. Kusimamia matumizi ya fedha .....	6.
2.3.Kusimamia ufanisi/utendaji .....	19
2.4.Kusimamia uadilifu wa umma .....	23 <b>Error! Bookmark not defined.</b>
2.5 Kusimamia mamlaka ya umma.....	24
SEHEMU YA TATU .....	28
3.1 Changamoto na Tulicho jifunza .....	28
3.2 Mapendekezo na Hitimisho.....	29
3.3 Marejeo .....	20

## **Vifupisho**

AP	Annual Plan
ARV	Ant Retroviral
CAG	Controller and Auditor General
CCHP	Council Comprehensive Health Plan
CHF	Community Health Fund
CSA	Centre for Social Accountability
DGP	Development Partner Group
FS	Forum Syd
GDP	Gross Domestic Product
JRF	Joint Revolving Fund
LGAs	Local Government Authorities
LAAC	Local Authorities Accounting Committee
MDAs	Ministries Departments and Agencies
MDC	Morogoro District Council
MOFEA	Ministry of Finance and Economic Affairs
MKUKUTA	Mpangowa Kupunguza Umaskinina Kukuzwa Uchumi Tanzania (National Strategy for Growth and Reduction of Poverty)
MMAM	Mpangowa Maendeleoya Afyaya Msingi (Primary Health Services Development Programme)
MTEF	Medium Term Expenditure Framework
MTSPBM	Medium Term Strategic Planning and Budgeting Manual (2005)
NAO	National Audit Office
NGO	Non – Government Organization
OPRAS	Open Performance Review and Appraisal System
PETs	Public Expenditure Tracking System
PMO	Prime Ministers' Office
PMO-RALG	Prime Ministers' Office Regional Authority and Local Government
PO-PSM	Presidents' Office Public Service Management
PF	Policy Forum
SAM	Social Accountability Monitoring
SP	Strategic Planning
STI	Sexual Transmission Infections
ToT	Training of Trainers
UNGONET	Ukerewe Non-Governmental Organizations Networking
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
VCT	Voluntary Councilling and Test
VVU	Virus Vya Ukimwi

## **Shukrani**

Forum syd inapenda kuwashukuru Policy Forum kwa jitihada zao kwa kushirikiana nasi katika kutekeleza ufuatiliaji wa uwajibikaji jamii katika wilaya ya Ukerewe kwa mwaka 2010/2011.

Pia inatoa shukrani kwa UNGONET kwa kuvumilia na kufanya ufuatiliaji wa mfumo wa uwajibikaji, inawashukuru halmashauri ya wilaya ya Ukerewe katika kufanikisha zoezi hili.

## Dibaji

Taarifa hii inalenga kutoa matokeo ya uchambuzi wa sekta ya afya katika halmashauri ya wilaya ya Ukerewe kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, kwa kutumia zana ya ufuatiliaji wa mfumo wa uwajibikaji katika kufanya ufuatiliai wa rasilimali za umma. Taarifa imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inaelezea utangulizi na taarifa za awali za mchakato wa ufuatiliaji wa sekta ya afya katika halmashauri. Pia inalezea shughuli kuu zilizofanywa na Forum Syd na Policy Forum katika kutekeleza ufuatiliaji wa mfumo wa uwajibikaji wilayani Ukerewe.

Sehemu ya pili ya taarifa, inatoa maelezo kwa kina juu ya uchambuzi wa sekta ya afya kwa kutumia hatua tano za mchakato wa ufuatiliaji uwajibikaji jamii ambazo ni:-

- Hatua ya 1:Upangaji na Kugawana Rasilimali (Uchambuzi wa Mipango Uchambuzi wa Sera, Kuunda Sera za Maendeleo na Sheria)
- Hatua ya 2:Kusimamia Matumizi (PETs Ufuatiliaji Taarifa za Matumizi ya Umma)
- Hatua ya 3: Kusimamia Ufanisi/utendaji (Kusimamia Utekelezaji malengo Miongozo ya Serikali za Mitaa)
- Hatua ya 4: Maadili ya Umma (Sheria za Kupambana na Rushwa Mfumo wa Maadili ya Umma, Viongozi na Watendaji
- Hatua ya 5:usimamizi wa Mamlaka (Jukwaa la Mijadala /Majadiliano Vyombo vya Habari, Kujadilika Sera kwa Jamii, Serikali na viongozi kufanyakazi na AZAKI

Sehemu ya tatu ya taarifa inaelezea matokeo ya uchambuzi yaliyopatikana toka ndani ya nyaraka za utendaji/ ufanisi wa mipango ya halmashauri kwa mwaka 2010/11. Kwa ufupi matokeo ya ufuatiliaji huu, ni kama kutokutumika kwa Mfuko wa afya wa jamii (CHF) kiasi cha TShs 29,780,000.00 zinaonekana hazikutumika ikiwa ni kama ni michango ya wananchi katika mifuko ya afya wa jamii. Pi iligundulika kiasi kikubwa cha fedha kilibaki 362,707,841.75 kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Kutokuwepo kwa mchango wa halmashauri katika bajeti ya afya ya wilaya.

Sehemu ya mwisho ya ripoti inaonesha changamoto na tulicho jifunza kutokana na utekelezaji wa zoezi hili ndani ya wilaya. Pia sehemu hi inatoa ushauri /maoni kutokana na matokeo yaliyoonekana katika uchambuzi huu ambayo yataboresha uwajibikaji katika halmashauri ambapo kwa upande mwengine utasaidia upatikananji wa huduma bora za kijamii ambayo ni msingi mkubwa wa haki za msingi za binadamu.

## **SEHEMU YA KWANZA**

### **1.0 Utangulizi**

Forum Syd ni mtandao wa zaidi ya asasi 200 za kiraia zilizoko Sweden yenye lengo la kupunguza umaskini, usawa na kuchochera demokrasia. Shirika la Forum Syd limepata ufadili kutoka Sida -Tanzania kutekeleza mradi wa **Uwajibikaji wa Kijamii** nchini Tanzania. Mradi huu unalenga vijiji na kata za Wilaya za Karagwe, Magu na Ukerewe. Mradi ulianza mwezi Mei 2010 ukiwa na lengo la kusaidia na kuimarisha jithada za wadau wa maendeleo kwa kuwajenjea uwezo kwa njia ya mafunzo mbalimbali. Walengwa wa mradi huu ni watu waishio na virusi vya Ukimwi (WAVIU), walemavu, wanawake na vijana. Mwezi Agosti 2012, PF kwa kwa kushirikiana na CSA waliwachagua wafanyakazi wawili wa Forum Syd kuhuduria Mafunzo ya ToT, baada ya kumaliza Mafunzo PF walishirikiana na FS katika kutekeleza kile walichojifunza. Katika kufanya utekelezaji wa mfumo wa uwajibikaji jamii walipendekeza kufanya ufuatiliaji huo na UGONET. Pia walipendekeza kufanya ufuatiliaji katika sekta ya afya katika halmashauri ya Ukerewe.

### **Makubaliano ya Forum Syd na Policy Forum**

Baada ya kuamua kufanya ufuatiliaji wa mfumo wa uwajibikaji jamii, FS waliandaa Mafunzo na mtandao wa asasi wa kiraia, malengo yakiwa ni:-

- Kujengea uwezo mtandao juu ya dhana ya SAM
- Kufanya ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa H/W ya Ukerewe hususani katika sekta ya afya
- Kuangalia ubora wa huduma zinazotolewa kwa kuzingatia haki za msingi za binadamu
- Kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika michakato ya maendeleo

Baada ya Mafunzo washiriki walichaguana timu ya utekelezaji ya wilaya ambayo iliwajibika katika kufanya uchambuzi wa mfumo wa uwajibikaji miongoni mwao. Timu hiyo ilikusanya taarifa, ilifanya uchambuzi, kufanya kikao cha mrejesho na washika dau na mwishoni wakaandaa mkakati wa uchechemuzi.

Taarifa zilizokusanywa zilikuwa ni Mpango Mahsusni wa Idara ya Afya (CCHP 2010/11), Mpango Mkakati wa H/W ya Ukerewe (SP) 2008/2011, MTEF 2010/11-2012/2013, Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango Mahsusni wa Idara ya Afya June 2011, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Muhtasari wa Kikao cha Baraza la Madiwani 25/6/2012, Muhtasari wa Kikao cha Baraza la Madiwani 30/1/2012, Taarifa ya CAG ya 2010/2011 kwa Halmashauri zote na Taarifa ya CAG ya H/W Ukerewe June 2011.

## **SEHEMU YA PILI**

### **2.0 Uchambuzi wa taarifa na matokeo**

#### **2.1. Mgawanyo wa rasilimali na Mpango Mkakati**

##### **2.1.1 Mambo ya kuzingatia/kuangalia katika Mpango na mgawanyo wa rasilimali**

Mgawanyo wa rasilimali na mpango mkakati ulio bora na unaozingatia mahitaji ya watu ni ule uliyotayarishwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali kwa kuzingatia vipaumbele vya jamii husika na bahasha ya rasilimali waliyonayo ili uweze kufikia mahitaji ya jamii.

Ukichukua dhana ya Muundo wa Matumizi ya Muda wa Kati– (MTEF) ambao kimsingi unaonyesha ni kwa jinsi gani maamuzi ya mgawanyo wa rasilimali utakavyowezesha kufikia Malengo ya sera ya serikali na kuweka mipaka katika matumizi na mapato yaliyokusanya kwa mwaka huo wa fedha.

Wizara ya Fedha (MOEFA) inawajibika kwa sera kubwa za uchumi, mifumo ya fedha na kodi .Matarajio makubwa ya kiuchumi yanapangwa kulinga na makadirio ya mapato amabayo ni :- Ongezeko la pato la Taifa (GDP), Makisio ya mfumuko wa bei, Kushuka kwa thamani ya fedha, Kiwango cha ubadilishanaji fedha katika kipindi cha miaka mitatu, Ongezeko la uingizaji wa bidhaa

Kikosi kazi cha maboresho ya kodi kinachoongozwa na Waziri uandaa mashauriano na wadau mbalimbali (Mwezi Februari) na kina wajibu wa kuunda sera ya kodi na kufanya mabadliko yoyote yatakayopendekezwa kuwemo ndani ya Muswada wa Fedha.

Mwongozo wa Mpango na Bajeti (PBGs) hutoa taarifa muhimu za awali za bajeti. Kwa nyongeza; kunanyaraka zingine 3 zinazoandaliwa ambazo pia uchangia taarifa zaidi kwenye PBGs , nyaraka hizo ni:- Mapitio ya ufanisi ya uchumi mkubwa uliopo,Mkakati mtambuka wa MTEF, Mapitio ya Maendeleo ya Fedha na Mpango wa Usimamizi wa Bajeti (ambao kwa sasa umebadilishwa kuwa PEFAR), Nyaraka hizi baadaye huwakilishwa na kujadiliwa na wadau na washauri mbalimbali wakati wa (PER) mwezi Mei. Taasisi lazima zitumie makisio ya mgawanyo na vipaumbele vya sera kama mwongozo Uwasilishaji wa bajeti shuruti utokane na taarifa toka ngazi ya chini-juu.

Idara zilizoko ndani ya serikali za mtaa (LGA) hujadili mipango na makadirio ya bajeti na kamati husika kwenye ngazi ya Halmashauri na sekretariati ya mkoa. Makadirio ya mwisho uwasilishwa ktk Baraza la madiwani kuitia Kamati ya Fedha. Baraza linapiga kura kuitisha au kutopitisha bajeti baada ya majadiriano. Bajeti ikitishwa huunganishwa kwenye Bajeti ya TAMISEMI kabla ya kupelekwa MOFEA pamoa na zile za MDAs.

MOFEA nao wanaweza kufanya mashauriano na wadau wengine (mfano, wabia wa maendeleo na sekta binafsi). Kuna fursa za majadiliano katika kipindi chote cha mchakato kati/ baina ya ngazi mbalimbali.

Kamati mipango ya bajeti ina wajumbe toka PMO, PMO-RALG, MOFEA, PO-PSM, na vipaumbele vya sekta za wizara vinatumia nyaraka za bajeti ya awali kusaidia uundaji wa kupanga bajeti.

### **Nyaraka zinazotayarishwa**

Ili kuhakikisha utekelezaji wa ugawaji rasilimali na upangaji mpango mkakati unakidhi vigezo, mameneja wanaitaji kutayarisha mipango ya kutoa huduma za kijamii na kutumia rasilimali ambayo itatoa mahusiano kati ya kimkoa na kitaifa. Pia wanatakiwa kujumlisha mipango muhimu ya kiprogramu katika ngazi tatu za serikali; utafutaji wa mikataba; ngazi ya mikataba ya huduma; ukarabati wa miundombinu na maendeleo ya mipango. Kwa kuongezea ugawanyaji wa rasilimali au nyaraka zinazotayarishwa ambazo zinazatoa ramani katika mpango mkakati katika ngazi ya chini, kitaifa na kimataifa. Nyaraka hizi ni; taarifa za sera ya bajeti; Matumizi ya Muda wa Kati wa miaka 3– (MTEF), makisio ya mapato na matumizi (yanayojumlisha utangulizi wa uchambuzi kijamii na kiuchumi yanayoandaliliwa na MTEF na mgawanyo wa bajeti; taarifa za kina kwa programu; taarifa za mapitio ya kina ya sasa ; taarifa za kina za uhamisho; na makadirio ya kina ya mapato ya ukarabati wa miundombinu.

### **Nyaraka zilizopatikana na matokeo ya Uchambuzi**

Kwa kuangalia mahitaji ya mgawanyo wa rasilimali na upangaji mzuri na nyaraka zilizoitajika kuandaliwa katika hatua hii, timu ya uchambuzi ilifanikiwa Kupata nyaraka kama vile:-mpango mkakati 2010/2011 na CCHP 2010/2011 ambazo zilitumika katika kufanya uchambuzi na ifuatavyo ni matokeo ya uchambuzi huo:-

- *Mchakato wa uandaaji wa Mipango***

Katika uchambuzi wa Mpango Mkakati timu ilibaini kuwa Halmashauri ina Malengo yafuatayo sita ya utekelezaji ambayo ni, Kuboresha huduma za jamii na Kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI,Kuboresha huduma za Jamii ziwe zenye na ubora na ufanisi, Huduma za Kiuchumi na miundombinu ziwe zenye ubora na kiwango, Huduma nzuri za uongozi na Utawala, Uhifadhi wa maliasili na utunzaji wa mazingira uimarishe na Kuwezesha Ustawi wa jamii Jinsia na kuinua jamii

Timu iliamua kufanya kazi lengo namba 1 na lengo 2 ambayo ni ***Kuboresha huduma za jamii na Kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI*** pamoja na ***Kuboresha huduma za Jamii ziwe na ubora na zenye ufanisi*** kwa sababu takwimu ya maambukizi ya UKIMWI/VVU ni kubwa kwa 12% ukilinganisha na takwimu za taifa ambazo ni 7% kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Halmashauri 2008/11, uk 16, pia muingilio mkubwa wa

wananchi kutokana na kambi za wavuvi ambazo husababisha maambukizi kwa kasi kubwa sana yanayochangiwa naufanyaji wa ngono zembe pamoja na unyanyapaa uliopo.

Pia timu iliona ni muhimu kufanya uchambuzi malengo haya kutokana na Idara ya afya kuwa na upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali ambao hupelekeea huduma kuwa hafifu. (CCHP 2010/11, uk 31), Upungufu mkubwa wa madawa uliopo pamoja na vitendea kazi, Miundombinu mibovu iliyopo katika utoaji huduma mfano, inapotokea mgonjwa kapewa rufaa kutoka zahanati au vituo vya afya kwenda hospitali ya wilaya, pia rufaa toka hospitali ya wilaya kwenda katika hospitali ya Bugando na Sekou Toure ni shida katika usafiri wa kumpeleka mgonjwa huyo.

**Katika lengo la Kuboresha huduma za jamii na Kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI** halmashauri ilipanga Kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI kutoka 12% hadi 7% ifikapo 2011 katika wilaya; kwa kuongeza Uhamasishaji wa jamii juu ya matumizi ya kinga, Kuhakikisha kuwa tunatumia damu salama tunapo hitaji kuongeza damu, shughuli zilizopangwa kufanyika ni pamoja na Kupima damu kwa mto damu, Kutoa mafunzo kwa HSPs 270 juu ya IPC, Kutoa elimu ya afya kwa vijiji 74 juu ya kuzuia maambukizi ya VVU/UKIMWI, Kutoa elimu kwa HSPs juu ya magonjwa ya zinaa (STI) pamoja na Kununua gari moja kwa ajili ya ufuutiliaji. Chanzo: Mpango mkakati 2008/2011 uk 17.

**Katika Lengo la Kuboresha huduma za Jamii ziwe na ubora na ufanisi** halmashauri ilipanga kujenga nyumba za madaktari, kuweka umeme katika zahanati ya Hamkoko na Murutunguru, kufundisha watu **kuhusu** (HSPs) Komputa Mwanza, Uhamasishaji juu ya mifuko ya afya ya Jamii (CHF), Utoaji wa mafunzo (OPRAS) kwa watumishi wapya walioajiriwa, Kufanya upimaji wa hiari na ushauri nasaha wa kuhamahama katika visiwa vidogo (VCT) na VVU/UKIMWI.

- ***Uundaji wa mpango mkakati wa halmshauri***

Mchakato wa kuandaa mpango mkakati wa miaka mitatu wa halmashauri kwa mwaka 2008/2011 haikushirikisha wadau mbalimbali. Nyaraka haionyeshi kama walishirikishwa kwa sababu taarifa ya Mwenyekiti wa Halmashauri na mkurugenzi mtendaji zote hazitaji wadau walioshirikishwa ambapo ni kinyume na katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na marekebisho ya mwaka 2005 ibara ya 146(1) na sheria za mamlaka ya Serikali za mitaa namba 7 kifungu namba 1(a),(b) na 8 kifungu namba 54 namba 1 (f) ya mwaka 1982 vipengele hivyo vinawataka mamlaka za Serikali za Mitaa kuwashirikisha wananchi katika kupanga mipango ya maendeleo na utekelezaji wake.

Mpango mkakati wa afya wa 2010/11(CCHP) unaonyesha wameshirikisha wadau katika kuaandaa Mpango wa Afya na kuwataja kwa majina na wanakotoka. Hivyo mpango huu ulifuata sheria na taratibu zilizowekwa. ( Mpango wa Afya , 2010/11

- ***Uchambuzi wa hali ya afya***

Matokeo ya uchambuzi wa huu yameonesha Wilaya ina Hospitali 1 ya serikali yeye vitanda 160. Pia ina vituo vitatu (3) vya Afya vyenye uwezo wa kulaza wagonjwa 18 hadi 20 kila kimoja. Aidha zipo zahanati 26, kati yake 23 ni za Serikali na 2 ni za kidini na 1 ni ya mtu binafsi. Yapo maduka 31 ya dawa baridi ya binadamu.

Magonjwa makuu yanayosumbua wakazi wa Wilaya ya ukerewe, kwa kuzingatia takwimu za kuugua na mahudhurio katika vituo vya huduma za afya, ni malaria ambapo Nyaraka inaonyesha vifo 73/4820 vinatokana na ugonjwa wa malaria amba unashika namba moja kati ya magonjwa kumi na asilimia 65 ya vifo vingine vinasababishwa na upungufu wa damu (Anaemia). (CCHP, 2010/2011).

Magonjwa mengine ni pamoja na kuharisha, kichocho/minyoo, homa ya matumbo, nimonia na magonjwa ya njia ya mkojo "Urogenital tract Infection" (UTI) pamoja na UKIMWI, kifua kikuu na macho. Chanzo cha taarifa: **CCHP 2010/2011, Uk 24 .**

Jedwali hilo hapo chini linaonyesha matatizo au changamoto kubwa ambazo ni Ugunjwa wa Malaria, UKIMW/VVU pamoja na Magonjwa ya moyo ambayo yanahitaji uangalizi wa juu katika sekta ya afya wilayani Ukerewe.

#### 1.1.Jedwali : wagonjwa wanaondikishwa na vifo

Ugonjwa	chini ya miaka 5		zaidi ya miaka5		jumla		CFR %
	andikish wa	vifo	andikish wa	vifo	andikish wa	vifo	
Kuharisha	675	5	797	31	1472	35	2.4
Malaria Sugu	492	31	400	21	892	52	5.8
malaria uncomplicated	2425	9	1503	12	3928	21	0.5
Kifua kikuu	1	0	71	4	72	4	5.5
Anaemia	459	40	499	25	958	65	6.7
Pneumomia	418	8	241	6	659	14	2.1
PID	0	0	95	0	95	0	0.0
Pregnancy complications	0	0	958	10	958	10	1

Snake or insect bites	8	0	5	1	13	1	7.7
burns	0	0	19	1	19	1	5.2
poisoning	5	0	36	1	41	1	2.4
Clinical AIDS	0	0	158	21	158	21	13.2
Cardiovascular diseases	0	0	39	6	39	6	15.4
Fractures	1	0	37	0	38	0	0
others diagnosis	28	0	3323	22	3351	27	0.8
III defined condition	4	0	336	1	340	1	0.2
Total diagnoses	4516	93	8517	161	13033	259	68.9

Chanzo: CCHP, 2010/2011

Uwiano wa watumiaji wa kituo cha afya ni 1:86943 na kwa zahanati ni uwiano wa 1:1003. Pia ilibainika katika mpango wa idara ya afya vifo vya wamama wajawazito ni 119/100,00 kwa wanaozaa na vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano ni 2/1000 na maambukizi makubwa ya virus vya UKIMWI ni asilimia 12 ambayo kimsingi yanazidi wastani wa maambukizi kitaifa, idadi ya watumiaji wa dawa za ARV wameongezeka toka 733 kwenda 1220 (CCHP, 2010/2011 ukurasa 1).

Pamoja na hayo Halmashauri inakabiliwa na matatizo ya kimfumo na uongozi ambayo kwanamna moja ama nyingine yanakwamisha utoaji bora huduma za Afya, matatizo hayo ni pamoja na Malipo ya chini kwa wahudumu wa afya, Mfumo mbaya wa mawasiliano, Watumishi wachache wanaopata mafunzo, Vyanzo vidogo vya mapato na Usimamizi usioridhisha wa ndani na nje.

- ***Idadi ya watumishi***

Kwa upande wa watumishi wa Afya timu ilibaini yafuatayo:

**Mahitaji ya Watumishi katika Wilaya ni 515. Waliopo ni Watumishi 272 hivyo kuna upungufu wa watumishi 243. (CCHP: 2010/2011 Uk 33-35**

Ukiangalia katika mpango wa CCHP 2010/2011 mahitaji ya watumishi ni 515 lakini katika taarifa ya utekelezaji wa mpango huo inaonyesha mahitaji ya watumishi ni 480. Vilevile taarifa hizi zimetofautiana pia katika idadi ya watumishi waliopo pamoja na upungufu wa watumishi uliopo, CCHP 2010/2011 watumishi waliopo ni 272

Wakati taarifa ya utekelezaji ya June 2011 inaonyesha watumishi waliopo ni 358, na upungufu CCHP 2010/2011 243 wakati kwenye taarifa ya utekelezaji ni 282 waliopo ni 272 na pungufu 243.

**Swali: Taarifa ipi ni sahihi kuhusiana na idadi ya watumishi waliopo katika idara ya afya?**

## MATOKEO

KADA	MAHITAJI	WALIOPPO	UPUNGUFU
Health Officer	24	10	15
Medical Attendant	74	10	64
Tabibu (Clinical Officer)	13	3	10
AMO	5	-	5
Lab technician	2	2	3
Clinical Laundrer	4	-	4
Medical Recorder	4	4	2

15

Chanzo: CCHP 2010/2011

Pamoja na halmashauri kuwa na upungufu mkubwa wa watumishi, haijaweka mpango madhubuti wa kuweka vivutio vya kubakiza wafanyakazi. Ukiangalia katika mpango wa CCHP 2010/11 vivutio viliyyowekwa ni kama, kununua sare za wafanyakazi, kutoa chai, kugharamia mazishi pamoja na posho. Ukubwa wa tatizo la upungufu wa watumishi, na mpango wa kubakiza watumishi bado hauendani kaika Kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi

Katika lengo la kupunguza maambukizi ya VVU, timu ilibaini yafuatayo:-

December 2009 idadi ya watu waliopimwa VVU ilikuwa ni 176,932 na Octoba 2011 idadi ilifikia 207,067 na lengo lilikuwa ni Kupunguza toka asilimia 12 mpaka asilimia 7. Taarifa inaonyesha maambukizi yamepungua mpaka asilimia 5.2 . Je?, idadi ya waliopimwa ni kigezo tosha cha kuonyesha maambukizi yamepungua. Idadi ya waliopimwa ni sawa na asilimia 79.3 ya wakazi wote wa Ukerewe. (260,831. Sensa: 2002).

Katika uchambuzi wa nyaraka kuna mkanganganyiko kati ya Mpango Mkakati na CCHP.

Lengo la kupunguza maambukizi toka asilimia 12 asilimia mpaka 7 linaonekana katika mpango mkakati wa mwaka 2008/2011 litafikiwa mwaka 2011, Lakini CCHP ya mwaka 2010/2011 katika lengo hilohilo inaonekana kuwa maambukizi ya VVU yatapungua toka 5.2% mpaka 5% June, 2013 (CCHP 2010/2011 Uk 3)

### **Swali: Inawezekanaje malengo yakafikiwa wakati taarifa mbili zenyenye lengo moja zinatofautiana?**

- **Miradi ya sekta ya afya inayotekelizwa katika wilaya ya Ukerewe**

#### **MPANGO WA MAENDELEO WA AFYA YA MSINGI (MMAM)**

Wilaya imeitikia agizo la Serikali<sup>1</sup> la kusogeza huduma za afya kwa kila kijiji kuwa na zahanati, na kata kuwa na kituo cha afya, kwa kuzingatia kuwa, kituo cha huduma kisizidi umbali wa kilometra tano kutoka kwa wananchi. Wilaya imeendelea kujenga nyumba za watumishi katika zahanati sita (6) za Muluseni, Bugula, Busangumugu, Hamkoko na Kaseni: CCHP Uk 24.

Lakini katika kutekeleza miradi hiyo timu ilibaini takribani miradi yote kutokamilika kwa asilimia 100, ambapo mradi wa nyumba za watumishi za Bugula haujakamilika ila unakizana na taarifa ya uekelezaji wa mpango mahususi wa afya CCHP, June 2012, nyumba iliyojengwa ni 2:1 ila haina milango, choo hakijamilika, singiboard haijawekwa na pia imejengw chini y kiwango.

#### **MGAWANYO WA RASILIMALI**


Katika mwaka wa 2010/11 jumla ya bajeti ya Halmashauri ilikuwa ni kiasi cha Tsh. 12,494,402,422/= **(CAG 15,539,867,511)** ambapo katika mgawanyo wa kisekta ilikuwa ni kama inavyoonekeka katika jedwali hapa chini:

<b>SEKTA</b>	<b>KIASI</b>	<b>ASILIMIA</b>
<b>MAJI</b>	83,236,309	0.666188795
<b>ELIMU</b>	6,243,315,602	49.9689012
<b>AFYA</b>	3,989,205,564	31.92794204
<b>KILIMO</b>	147,520,133	1.180689784
<b>MIUNDOMBINU</b>	67,577,405	0.540861441
<b>MENGINEYO</b>	1,963,547,409	15.71541673
<b>JUMLA</b>	12,494,402,422	100

<sup>1</sup> Sera ya afya ya mwaka 2007

## Jedwali 1: Mgawanyo kwa sekta, Chanzo Taarifa ya Mapato na Matumizi

Hapa chini ni jinsi mgawanyo huu unavyoonekana kwenye pie chart katika asilimia. Ambapo jumla ya bajeti ya halmashauri elimu iliongoza kwa kupata asilimia 50% ikifuatiwa na afya iliyopata 32% ambayo inaonyesha afya imekuwa kipaumbele namba mbili katika bajeti kwa mwaka huo wa fedha.



## Mchoro 1: Mgawanyo kwa sekta, Chanzo CCHP 2010/11 uk 4.


Bajeti ya sekta ya afya pekee, matumizi katika mishahara (PE) ilikuwa ni 60%, matumizi ya maendeleo (DE) ni 34% wakati matumzi mengineyo (OC) ilikuwa ni 6%. Kama ionekanavyo hapa chini:

<b>MISHAHARA (PE)</b>	<b>2,377,262,264.00</b>
<b>MATUMIZI YA KAWAIDA (OC)</b>	<b>236,788,500.00</b>
<b>MATUMIZI YA MAENDELEO(DE)</b>	<b>1,375,149,800.00</b>
<b>JUMLA</b>	<b>3,989,200,564.00</b>

## Jedwali 2: Mgawanyo katika sekta ya Afya, Chanzo CCHP 2010/11

## MGAWANYO - AFYA

- MISHAHARA (PE)
- MATUMIZI YA KAWAIDA (OC)
- MATUMIZI YA MAENDELEO(DE)



Mchoro 2: Mgawanyo katika sekta ya Afya, Chanzo CCHP 2010/11

### 2.2 USIMAMIZI WA MATUMIZI

#### **Mambo ya kuzingatia/kuangalia katika usisimamizi wa fedha**

Hatua ya pili katika kutekeleza mfumo wa uwajibikaji jamii ni usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Pindi bajeti inapogawanywa kwa mamalaka za serikli kwa ajili ya kutekelez shughuli ambazo zimebainishwa kwenye mpango mkakati, kwa sababu hiyo kuna haja ya kufuatilia matumizi kuangalia kama halmashauri imetekeleza bajeti na mipango yake kama ilivyopangwa. Kufuatilia hili, taarifa za fedha zaitajika kutayarishwa na mameneja na wasaidizi katika kufuatilia matumizi ya fedha na bajeti iliyopitishwa.

#### **Nyaraka zilizotayarishwa**

Ili kuhakikisha utekelezaji wa usimamizi wa matumizi ya fedha unakidhi vigezo, kuna nyaraka ambazo zinatakiwa kutayarishwa n mameneja na watumishi, nyaraka hizi ni pamoja na taarifa za fedha za mwezi, taarifa za fedha za robo mwaka, taarifa za mwaka za mapato na matumizi, taarifa za ukaguzi ya mwaka na taarifa ya ukaguzi wa ndani.

#### **Nyaraka zilizopatikana**

Nyaraka ambazo timu ilifanikiwa kuzipata na kuzitumia katika mchakato huu wa uchambuzi ni pamoja na ripoti ya utekelezaji wa idara ya afya (CCHP) kwa mwaka 2010/2011 na ripoti ya mkaguzi na mdhibiti mkuu wa serikali ya mwaka 2010/2011


Matokeo ya Uchambuzi uchambuzi ulibaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 halmashauri ya Ukerewe kuititia idara ya afya walitumia zaidi ya kilichopangwa katika ruzuku ya mishahara. Pia nyaraka zinaonyesha kuwa Kiasi kikubwa cha fedha kilibaki ambapo takribani Tshs 362,707,841.75. Kutokuwepo kwa mchango wa halmashauri katika bajeti ya afya ya wilaya ambapo hupelekea halmashauri kutotimiza Malengo yake ya sekta

ya afya na kukiuka haki za msingi za binadamu. Kutoikutumika kwa Mfuko wa afya wa jamii (Community health fund-CHF) Shilingi 29,780,000.00. Pia uchambuzi uligundua kuwa katika bajeti fedha nydingi za afya zinakuwa Backlog (Bakaa) mfano .2009/2010.

### **JUMLA YA FEDHA ZILIZOIDHINISHWA na ZILIZOTUMIKA :-**

Katika mwaka huo wa bajeti, timu ilibaini kwa miaka mitatu mfululizo halmashauri ilikuwa ikipokea kiasi cha fedha pungufu na kile walichokisia, na pia iliweza kutumia pesa yote kama inavyoonekana katika jedwali au imekuwa ikitumia bajeti yote bila bakaa

### **JUMLA YA MAPATO NA MATUMIZI**



Mchoro3: Mapato na matumizi H/W Ukerewe, Chanzo Taarifa ya Mapato na Matumizi

### **Timu ilibaini yafuatayo:-**

- Kiasi kikubwa cha fedha kilibaki ambapo takribani Tshs 279,524,538.75 (CCHP ripoti Uk 2).
- Pia kutokuwepo kwa mchango wa halmashauri katika bajeti ya afya kwa mwaka huo wa fedha.
- Halmashauri tokea mwaka 2008/09 hadi 2010/11 walikuwa wakipata pungufu ya karibia 25% ya fedha waliyokuwa wanaomba, hata hivyo walikuwa wakitumia pesa yote kama ilivopokelewa. Hii yawezekana vipi kutumia mpaka shilingi ya mwisho bila salio.
- Kutotumika kwa Mfuko wa afya wa jamii (Community health fund-CHF) Shilingi 29,780,000 ambazo zilichangwa toka kwa wananchi wa wilaya ya Ukerewe.

- Pia idara iliitumia zaidi ya kilichopangwa katika ruzuku ya mishahara kiasi cha Tshs 25,602,976.74 (CCHP Ripoti Uk 1) lakini Taarifa haioneshi sababu za kuzidi kwa matumizi ya mishahara, kama walionegeza wafanyakazi au la na kama ilikuwepo kwenye mpango.

### ***Uchambuzi wa taarifa ya jumla ya CAG kwa Halmashauri zote***

Katika ripoti ya CAG ya mwaka 2010/11 ilibainisha mambo mbalimbali yanayohusiana na usimamizi wa rasilimali kama ifuatavyo:-

- Wilaya ya ukerewe ilikuwa ni moja ya wilaya ambazo ina watumishi wasiochangia katika mifuko ya jamii ambapo jumla ya watumishi 182 hawakuwa wakichangia katika mfuko huu. Idadi ambayo ni kubwa ukilinganisha na wilaya nyingine zilizochukuliwa kama sampuli ambazo ni lleje yanye jumla ya watumishi 43 na Mbozi watumishi 141 wasiochangia. Hii inamadhara kwa watumishi hao kwani watakosa mafao yao wakati wa kustaafuli, hawatapata huduma za afya na pia mapato ya serikali kupungua kutokana na kutokatwa kodi ya mapato<sup>2</sup>.
- Vilevile kiasi cha shilling 12,831,520 kilikusanywa na vituo vya afya na zahanati katika halmashauri za wilaya ya Manyoni na Ukerewe lakini kiasi hicho cha fedha hakikuwasilishwa kwa mtunza fedha wa halmashauri. Kati ya hizi kiasi gani kinaihusu halmashauri ya wilaya ya Ukerewe<sup>3</sup>
- Uwasilishaji wa taarifa za fedha ulionyesha kwamba jumla ya matumizi katika halmashauri ya Ukerewe ni shs 11,237,985,118 lakini katika taarifa hiyo kulikuwa na jumla ya makosa katika malipo pungufu kiasi cha Tshs 1,191,188,161 na malipo ya zaidi kiasi cha Tshs 1,380,441,123
- Halmashauri ya wilaya ya Ukerewe imekuwa ikipata kwa mfululizo hati yenyeye shaka kwa kipindi cha mwaka 2007/08 hadi 2009/10 isipokuwa kwa mwaka 2010/11 ilipoweza kupata hati inayoridhisha. Hii inamaanisha kwamba halmashauri iliongeza ufanisi. Hata hivyo halmashauri ilikuwa na hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa zenye jumla ya shiliingi 3,691,167,767.<sup>4</sup>
- Halmashari ilishindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kiasi cha 10.4% ambapo ilipanga kukusanya kiasi cha shilling 860,000,000 ikafanikiwa kukusanya 770,596,512 ambayo ni tofauti ya kiasi cha shilingi 89,403,488<sup>5</sup>. ambapo

---

<sup>2</sup> *Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikal Ripoti Kuu ya Mamlaka ya Serikali za mitaa 2010/11 uk 102*

<sup>3</sup> Ibid uk 25

<sup>4</sup> Ibid uk170,172&191

<sup>5</sup> Ibid uk 196

shilingi 770,596,512 ambazo ni mapato ya ndani ya halmashauri zilichangia matumizi ya kawaida ya halmashari sawa na 6%<sup>6</sup>

- Vilevile katika CAG ripoti ilibaini kuwa Halmashauri ya wilaya ya Ukerewe kwa upande wa matumizi ya kawaida ilitumia pungufu kwa kiasi cha shilling 456,986,833 sawa na 3.9% ya shilingi 11,694,971,951<sup>7</sup>
- Halmashauri ilikuwa na ruzuku ya maendelo ya shilling 4,315,759,415 ambapo iliweza kutumia shilingi 2,449,881,843 na kiasi cha shilingi 1,865,877,572 sawa na 43.23% ya fedha zilibaki<sup>8</sup>. Pia katika fedha za mfuko wa jimbo kiasi cha shilingi 60,246,012 zilikuwa bakaa.
- Tathmini ya mifumo ya uthibiti wa ndani na masuala ya utawala bora katika halmashauri ya Ukerewe kwa muujibu wa CAG inaonesha kwamba halmashauri ina utendaji wa ukaguzi wa ndani usioridhisha kulingana na mfumo wa utoaji taarifa unaokubalika, pia ina mapungufu katika udhibiti wa teknolojia ya habari na mazingira, kutokuwepo kwa ufanisi wa utendaji kazi wa kamati ya ukaguzi, pia kutokuwepo kwa mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi na mapungufu katika mfumo wa kiuhasibu.ila kwa mujibu wa tathmini hiyo halmashauri ilionekana kuwa na mpango wa kimaandishi wa kuzuia udanganyifu na mfumo wa kiuhasibu unaotumia komputa.<sup>9</sup>
- Katika CAG ripoti, halmashauri ya ukerewe ilikuwa na masuala yasiyoshughulikiwa katika suluhisho za kibenki ambapo kiasi cha shilingi 43,275,135 ni mapokezi katika daftari la fedha ambayo hayamo benki, hundi ambazo hazikupelekwa benki ni kiasi cha shilingi 92,211,219, malipo yaliyofanywa na benki na hayamo katika daftari la fedha ni shilingi 4,949,095na mapokezi benki ambayo hayamo katika daftari la fedha ni shilling 22,227,678. Hata hivyo halmashauri haikuwa na kiasi chochote cha fedha ambacho hakikupelekwa benki.<sup>10</sup>hata hivyo kiasi cha masurufu ya shilingi 48,102,382 hayakurejeshwa hazina.
- Kukosekana kwa nyaraka zinazohusiana na umiliki wa mali za kudumu: kwa halmashauri ya Ukerewe – kukosekana kwa hati miliki, kadi za usajili na kitabu cha safari za magari . ukaguzi wa utaratibu uliifanyika kwenye baadhi ya mali za kudumu zilizochaguliwa na kugundua kwamba majengo yote yanayomilikiwa na halmashauri

---

<sup>6</sup> Ibid uk 200

<sup>7</sup> Ibid uk204

<sup>8</sup>Ibid 206

<sup>9</sup> Ibid 210

<sup>10</sup> Ibid 215

yenye thamani ya Shiling 19, 282,908,655 hayana hati ya miliki na magari yenyethamani ya shilingi 428, 714,352 kati ya shilingi 828,213,975 hayana kadi za usajili na vitabu vya safari ili kuhalalisha umiliki wa mali hizo. Jumla kuu ni shilling 19, 711,663,007.<sup>11</sup>

## **2.3. USIMAMIZI WA UFANISI/UTENDAJI**

### **Mambo ya kuzingatia/kuangalia katika usisimamizi wa fedha**

Hii ni hatu ya tatu ya utekelezaji mfumo wa uwajibikaji jamii, mara baada ya kupitishwa kwa bajeti utekelezaji wa bajeti hiyo uanza mara moja. Kasma inaitaji kuendeleza mipango inayoadhimiwa na kuiwezesha serikali kutekeleza mipango yake kwa ufanisi kwa kipindi cha mwaka mzima. Nyaraka kama vile, mipango ya utekelezaji ya mwaka, mipango ya ukaguzi wa ndani ya mwaka, na mipango ya manunuvi ya mwaka, ambayo kimsingi zinatayarishwa na matumizi yake mara baada ya mgawanyo wa bajeti unapopokelewa.

Mfumo wa kusimamia Ufanisi/utendaji nchini Tanzania unaanza na kwa utekelezaji wa mpango mkakati. Wakati mpango unatekelezwa, mifumo ya ndani nayo inatakiwa iwepo ili kuhakikisha kuwa malengo, shabaha na shughuli zinafanyika kwa kiwango kikubwa cha ufanisi na chenye ubora na kiuchumi. Mhasibu ana majukumu ya mwisho ya utekelezaji ya mpango mkakati katika kasma. Sheria nazo zinaitajika katika kuhakikisha kuwa mifumo ya ndani ipo na inahakikisha kuwa yanafanyika matumizi ya rasilimali na yanafanyiwa utekelezaji na mkaguzi wa ndani. Kitengo hiki cha ukaguzi wa ndani kinaangaliwa na kamati ya ukaguzi ambayo ukutana mara 4 kwa mwaka. Kitengo kinatayarishwa ripoti ya ukaguzi wa ndani kila mwisho wa mwaka ambayo uwasilishwa kwa mhasibu na nakala kwa ofisi ya ukaguzi ya taifa .

Ufutiliaji unafanywa na watu na kuna mfumo wa kufanya ufutiliaji wa ufanisi kwa watumishiwa umma ambao unaangaliwa na mhasibu kwa msaada wa usimamizi toka idara ya utumishi. Mchakato wa kusimamia ufanisi/utendaji wa mtu mmoja mmoja kwa watumishi wa serikali unaitwa Open Performance Review and Appraisal System (OPRAS). Mfumo huu unawahitaji watumishi wa umma kusaini makubaliano ya ufanisi kila mwaka. Pia OPRAS inafanyiwa mapitio katika kipindi cha katikati ya mwaka na mwisho wa mwaka kila kila mtumishi wa umma.

Taarifa za OPRAS zinakusanywa katika mfumo wa taarifa za taasisi kwa kila kitengo. Taarifa za robo mwaka zinaitajika kwa kipindi cha kwanza cha robo na cha tatu. Katika kipindi cha mwaka huo wa fedha taasisi za serikali ni lazima zitayarische taarifa ya mapitio ya nusu mwaka. Taarifa hizi zinaonyesha taarifa za ufanisi za mwaka ambazo zinapelekwa ofisi ya mkaguzi na mdhibiti mkuu wa hesabu na taarifa ya fedha kwa mwisho wa mwaka wa ukaguzi. Taarifa ya ufanisi ya mwaka inajumlisha utekelezaji wa shughuli na matokeo yake na baadaye inaalishwa kwa wizara husika ya fedha na taasisi na kwa mkuu wa mkoa kwa mamlaka ya serikali za mitaa na kusomwa na kupitishwa kwa kamati.

---

<sup>11</sup> Ibid 230

## **Nyaraka zilizotayarishwa**

Ili kuhakikisha utekelezaji wa mchakato wa usimamizi wa ufanisi au utendaji taarifa mbalimbali zinatakiwa ziandaliwe kama taarifa za ufanisi wa fedha, na taarifa za ufanisi wa fedha mwisho wa mwaka kwa kawaida zinajumlisha ukaguzi wa ufanisi na fedha , taarifa ya utekelezaji ya mpango biashara, taarifa za utafutaji watoa huduma, mikataba ya ufanisi kwa mameneja na taarifa za miundombinu na marekebisho.

### **Nyaraka Zilizopatikana**

Timu ilifanikiwa Kupata taarifa ya idara ya afya utekelezaji ya mwaka 2010/2011 na haya ni baadhi ya mambo yaliyogundulika.

### **Matokeo ya uchambuzi**

#### ***Timu ilibaini yafuatayo:-***

- Mahitaji walio baini hayakuendana na maeneo yaliyo kusudiwa katika sekta ya afya Mfano. Walisema wataweka umeme katika zahanati ya Hamkoko na Murutunguru. Katika taarifa ya utekelezaji ya mpango wa afya kwa mwaka huo inaonesha umeme kuwekwa katika zahanati ya muhula na Bukonyo (rejea CCHP ukurasa wa 3 na taarifa ya utekelezaji CCHP ukurasa 2
- Katika mpango wa afya CCHP 2010/2011 ukrasa 3 inaonekana itaji namba 4 ilikuwa ni Uhamasishaji juu ya mfuko wa afya ya jamii lakini katika taarifa ya utekelezaji ya mpango wa afya mwaka huo inaonesha kuwa hitaji hilo halikufanyiwa kazi kwa kutokuwa na shughuli/bajeti yoyote iliyotengwa kwa lengo hilo.
- Utoaji wa mafunzo ya (OPRAS) kwa watumishi wapya walioajiriwa, Haionyeshi shughuli kwamba itafanyika lini na watu wangapi . CCHP ukr 3
- Suala lingine tulilibaini si jema katika utekelezaji wa CCHP 2010/2011 sehemu 9 ukurasa 134 ni pamoja na shughuli zilizopangwa- ni 206; zilizotekelzwa ni 146.Rejea taarifa ya utekelezaji wa afya ya mwaka 2010/2011 ukurasa wa 134. Pia ufuatiliaji iligundua kuwa kuna shughuli zilizotekelzwa kwa kiwango cha kawaida- 59 ni sawa na 28% ya shughuli zote. Na kuna shughuli zilizotekelzwa bila kuwepo kwenye mpango wa – 124 ambayo ni 92% ya shughuli zote. Na shughuli ambazo hazikutekelezwa –shughuli 11 ambayo ni 8% ya shughuli zote.

jedwali: Hizi ni baadhi ya shughuli zilizotekelezwa kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa sekta ya afya ya mwaka 2010/2011 na kile kilichopangwa katika CCHP ya mwaka 2010/2011, kiambatanisho namba 7 ya taarifa ya utekelezaji wa CCHP June 2011

Na .	shughuli	Bajeti	Asilimia	Kasma	pesa iliyotumika	Asilimi a	remarks
14	Kuwezesha mafunzo ya siku 10 kwa watumishi 6 ifikapo june 2011	16,500,000/=	100%	CO1S0 5	12,869,500/=	100%	Bakaa haikuonyeshwa katika taarifa ya utekelezaji
15.	Kuwajenge a uwezo watumishi 3 wa HSPs hadi june 2011.	BF 3,750,000/=	100%	CO1S0 6	1,440,000/=	100%	Bakaa haikuonyeshwa katika taarifa ya utekelezaji
20	Kusafirisha wagojwa wenyе rufaa kutoka Nansio hadi Sekoutoure na Bugando,	BG 625,000/=	100%	CO210 6	625,000/=	100%	
9	Kuajili watoa huduma 3 wa kada	BG 1,798,600/=	100%	BO2S0 4	1,296,500/=		Backlog activity 2009/10

	mbalimbali uk 85						
5.	Manunuzi ya OLs drugs june 2011.	BF 504,000/=	AO1SO 1	100	504,000/=	100	

Pia timu ilibaini kuwa kuna upungufu wa umakini katika uandaaji wa taarifa za utekelezaji

- Kiambatisho 7 shughuli ya . 6 ya kuajiri watumishi 7, fedha tengwa ni 1,780,000/= ( Block Grant) fedha iliyopokelewa ni 2,873,155 na shughuli imeripotiwa kukamilika kwa 100%. Lakini jumla ya watumishi walioajiriwa ni 5 na fedha iliyotumika ni 1,373,155/=
- Hii ina maana kwamba shughuli hii haikukamilika kwa 100% na halmashauri ilitumia pungufu kwa Tshs 1,500,000/= Kiasi ambacho kingeweza kutumika kuajiri watumishi 2 waliobaki.
- Kiambatanisho 7 shughuli ya 8, imeonyesha kuwa kiasi cha Tshs 268,000/= zilitumika kugharamia mazishi, Lakini katika kiambatanisho cha 5 imeonyeshwa hakukuwa na kifo chochote cha mfanyakazi
- Shughuli ya 28 kuajiri watumishi 10 wa kada mbalimbali, lakini taarifa inaonyesha wameajiriwa watumishi 17 na shughuli imefanyika 100% badala ya zaidi. Pia bajeti iliyotengwa ni 3,740,000/= pesa iliyopokelewa na kutumika Shs 2, 575,000 (CCHP ripoti ukr 13 & 92)
- Shughuli ya 19 kuajiri watumishi 6 wa kada mbalimbali ambapo watumishi 7 walijiriwa lakini uk 115 bajeti ilikuwa 2,100,000/= lakini H/W haikupata pesa kwa shughuli hiyo.

*Swali:* Je, waliwezaje kuajiri watumishi 7 bila bajeti kama ilivyoripotiwa (CCHP ripoti Uk 32 )

## 2.4 Usimamizi wa uadilifu wa Umma

### Mambo ya kuzingatia/kuangalia katika usimamizi wa uadilifu

Usimamizi wa uadilifu ni hatua ya nne ya ufuatiliaji mfumo wa uwajibikaji wa umma. Mfumo wa usimamizi uadilifu ni lazima ujumuushe vyombo vya maamuzi, sheria na mifumo inayosimamia uadilifu. Hii ni lazima iambatane na huundwaji wa sheria na kanuni za ufanisi, kanuni za utumishi, utumishi mbovu, rushwa na maamuzi yanamnufaisha mtu mmoja.

Menaja na wafanya maamuzi ni lazima wahakikishe usimamizi wa uadilifu wa umma unalindwa ndani ya wizara au idara kwa pamoja na kuchukua hatua madhubuti pale ambapo kuna ubadhirifu wa matumizi mabaya ya rasilimali za umma. Kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma ya mwaka 2002 ilipendekeza kuanzishwa tume ya utumishi ya umma yenye jukumu la kuangalia usimamizi wa rasilimali watu katika taisisi za serikali. Hii inajumlisha kanuni za kinidhamu, utunzaji na uandikishwaji wa kesi za kinidhamu, taarifa za kuajiri, usimamizi wa ufanisi na mishahara na nyinginezo.

Zana ya kupima mfumo wa usimamizi wa ufanisi hapa Tanzania unatumia OPRAS. Kwa mujibu wa MTSPBM, OPRAS inatoa wigo kwa SP, mpango kazi na bajeti kwenye ngazi ya mtu. Watumishi wote wanaitaji kusema wanachotegemea, watafanyaje kazi, na kwa jinsi gani wataboresha kazi zao. OPRAS ni mchakato unaosaidia kufikia haya mahitaji kwa kuboresha mahusiano kati ya meneja na walioko chini yake. Pia katika kuhakikisha kwamba uadilifu wa umma unasimamiwa ipasavyo mionganoni mwa watumishi wa umma, mameneja wote, wajumbe wa vyombo vya maamuzi na watumishi wa serikali kuu wanaitajika kutoa maelezo ya mali zao binafsi wanazomiliki.

### **Nyaraka zinazotayarishwa**

Ili kuhakikisha utekelezaji wa mchakato wa usimamizi wa uadilifu wa umma taarifa Zifuatazi zinatakiwa kuandaliwa; taarifa ya mkaguzi na mdhibiti mkuu wa mahesabu ya Serikali (hesabu, ufanisi na ukaguzi maalumu), taarifa za kinidhamu zilizochukuliwa kutokana na kesi za utovu wa nidhamu, taarifa za kinidhamu zilizochukuliwa kutokana na kutowajibika na uandikishwaji wa maslahi binafsi kwa mameneja na wafanya maamuzi. Timu ya ufuutiliaji ilifanikiwa kupata taarifa ya mkaguzi na mdhibiti mkuu wa mahesabu ya mwaka 2010/2011.

### **Timu ilibaini yafuatayo:-**

- H/W ina jumla ya watumishi 182 wasiochangia mifuko ya jamii hii inamadhara kwa watumishi hao kwani watakosa mafao yao wakati wa kustaaifu, hawatapata huduma za afya na pia mapato ya serikali kupungua kutokana na kutokatwa kodi ya mapato.
  - Vilevile kiasi cha shilling 12,831,520 kilikusanywa na vituo vya afya na zahanati katika H/W ya Manyoni na Ukerewe lakini kiasi hicho cha fedha hakikuwasilishwa kwa mtunza fedha wa halmashauri. Kati ya hizi kiasi gani kinaihusu halmashauri ya wilaya ya Ukerewe.
- 
- Tathmini ya mifumo ya uthibiti wa ndani na masuala ya utawala bora katika halmashauri ya Ukerewe kwa muujibu wa CAG inaonesha kwamba halmashauri ina utendaji wa ukaguzi wa ndani usioridhisha kulingana na mfumo wa utoaji taarifa unaokubalika,
  - Pia ina mapungufu katika udhibiti wa teknolojia ya habari na mazingira, kutokuwepo kwa ufanisi wa utendaji kazi wa kamati ya ukaguzi.

- Kutokuwepo kwa mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi na mapungufu katika mfumo wa kiuhasibu ila kwa mujibu wa tathmini hiyo halmashauri ilionekana kuwa na mpango wa kimaandishi wa kuzuia udanganyifu na mfumo wa kiuhasibu unaotumia komputa.

## 2.5 Usimamizi wa Mamlaka

### Mambo ya kuzingatia/kuangalia katika usisimamizi wa mamlaka

Usimamizi wa mamlaka hii ni hatua ya tano ya utekelezaji mfumo wa uwajibikaji jamii. Ukaguzi wa kujitegemea unafanywa na taasisi ya ukaguzi ni lazima ufanyike katika kila wizara au idara au mamlaka ya serikali za mitaa na kwa ufanisi. Kamati za kudumu za bunge na kamati za baraza la madiwani ni lazima wajadili taarifa za mwaka za wizara au idara au taarifa za serikali za mitaa na hoja za taasisi ya ukaguzi, inayojumlisha mambo ya msisitizo na mapendekezo yanayoonyesha hatua zilizochukuliwa. Kamati hizi ni lazima zitoe mapendekezo kwa mkuu wa wizara au idara au mamlaka za mitaa ili kuboresha usimamizi wa fedha na ufanisi ili kusaidia upatikanaji wa huduma za kijamii. Kamati hizi ni lazima zifanye ufuutiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo na hatua zilizochukuliwa kutokana na uchambuzi wa taasisi ya ukaguzi.

### Nyaraka zinazotayarishwa

Ili kuhakikisha utekelezaji wa mchakato wa usimamizi wa mamlaka taarifa mbalimbali zinatakiwa ziandaliwe kama taarifa za mwaka za wizara au idara au mamalka za mitaa, taarifa ya mkaguzi na mdhibiti mkuu wa hesabu za serikali na kamati za mamlaka na mihtasari inayojumlisha kamati za bunge na baraza, kamati ya mamlaka za mitaa za hesabu, mapendekezo na hatua za bunge na madiwani. Timu ya ufuutiliaji ilifanikiwa Kupata taarifa ya mkaguzi na mdhibiti mkuu wa hesabu ya mwaka 2010/2011, hoja za kujibu za mkaguzi na mdhibiti mkuu wa hesabu mwaka 2010/2011 na maoni ya mkaguzi wa ndani wa mahesabu kuhusu mifuko ya jamii ya afya kwa mwaka 2010/2011.

### Timu ilibaini yafuatayo:-

- H/W imekuwa ikipata kwa mfululizo hati yenyе shaka kwa kipindi 2007/08 -2009/10 isipokuwa kwa mwaka 2010/11 ilipoweza kupata hati inayoridhisha. Hii inamaanisha kwamba halmashauri iliongeza ufanisi.
- Hata hivyo halmashauri ilikuwa na hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa zenyе jumla ya shiliingi 3,691,167,767
- Halmashauri ilishindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kiasi cha 10.4% ambapo ilipanga kukusanya kiasi cha shilling 860,000,000 ikafanikiwa kukusanya 770,596,512

- Halmashauri ilikuwa na ruzuku ya maendelo ya shilling 4,315,759,415 ambapo iliweza kutumia shilingi 2,449,881,843 na kiasi cha shilingi 1,865,877,572 sawa na 43.23% ya fedha zilibaki
- Pia katika fedha za mfuko wa jimbo kiasi cha shilingi 60,246,012 zilikuwa bakaa
- Katika CAG ripoti, H/W ilikuwa na masuala yasiyoshughulikiwa katika suluhisho za kibenki ambapo kiasi cha shilingi 43,275,135 ni mapokezi katika daftari la fedha ambayo hayamo benki,
- Hundu ambazo hazikupelekwa benki ni kiasi cha shilingi 92,211,219, malipo yaliyofanywa na benki na hayamo katika daftari la fedha ni shilingi 4,949,095 na mapokezi benki ambayo hayamo katika daftari la fedha ni shilling 22,227,678.
- Kukosekana kwa hati miliki, kadi za usajili na kitabu cha safari za magari :-
- Majengo yanayomilikiwa na halmashauri yenyе thamani ya Shiling 19, 282,908,655 hayana hati ya miliki
- Magari yenyе thamani ya shilingi 428, 714,352 kati ya shilingi 828,213,975 hayana kadi za usajili na vitabu vya safari ili kuhalalisha umiliki wa mali hizo.

#### **Maoni ya Baraza kutokana na Hoja za mkaguzi mkuu na mdhibiti za mwaka 2010/2011**

- Mishahara iliyolipwa kwa watumishi waliostaafu na kufa kiasi cha Tshs 17,789,950 kikao cha baraza la Madiwani cha terehe 25/06/2012 agenda namba 2 Kilishauri menejimenti ifanye mawasiliano kusudi makato haya yarejeshwe hazina na pia walisisitiza upitiaji wa pay roll ufanyike kwa makini ili kuondokana na hoja hii killa mara.
- Ofisi ya Mganga mkuu isimamie utunzaji wa kumbukumbu muhimu za kifedha pia kusambaza kadi za wanachama rejista na risiti za kukusanya mapato kama ilivyoanishwa kwenye mwongozo. 3.2.1(CHMT)Role & Responsibility.
- Ununuzi wa Bajaji za Wagonjwa. Baraza lilishauri kuwepo na mawasiliano na Mkoa kusudi Bajaji hizo ziweze kununulia kwa sababu fedha zake ni za Muda mrefu.
- Taratibu za manunuzi zifuatwe kama zilivyoainishwa kwenye sheria ya manunuzi ya mwaka 2004.
- Katika kufanya uchambuzi ilibainika kuwa kulikuwa na uchereweshaji wa ukamilishaji wa jengo la upatikanaji wa kituo cha Afya Bwisya-Ukara 64916960.00. Mkataba :UDC/CDC/201-2011 wa tarehe 24/12/2010-07/05/2011. Alikatwa shilingi 38,950,440.00

### **Maoni ya mkaguzi wa ndani kuhusu taarifa ya mfuko wa afya ya jamii(CHF)**

- Kata pamoja na kamati za afya,zahanati,kituo cha afya zitumie fedha kwa kuagiza manunuzi ya vifaa,tiba,dawa kwa kuzingatia bajeti na pia taratibu za manunuzi zifuatwe.
- Kutokutolewa kwa kadi za uanachama pamoja kukosekana kwa rejista ya mwanachama katika vituo vya afya na zahanati .
- Vituo vya afya /Zahanati viwe vimeweka kumbukumbu kwa kuwaandikia wanachama waliopata huduma kwenye rejista maalum ambayo itakaguliwa

**Swali: ni kwa kiasi gani haya yote yameteklezwa?**

### **Maoni ya jumla ya mkaguzi wa ndani.**

- Utaratibu wa vikao katika kata pamoja na kamati za afya ya zahanati wakae na waandike maombi ya ununuzi wa dawa kwa ajili ya wanachama.
- 60% ya fedha iliyokusanywa iende kwenye ununuzi wa dawa na pia ziwe zinawasilishwa mara moja kama utaratibu ulivyo kabla ya kutuma maombi ya ununuzi wa dawa kutoka zahanati/vituo vya afya

### **Sehemu ya tatu**

#### **Changamoto na tulichojifunza**

#### **Muda na Upatikanaji wa baadhi ya nyaraka za serikali**

Upatikanaji wa nyaraka za serikali ulikuwa wenye changamoto kwa kiasi kidogo, kwani nyaraka nyingine hazikujulikana zilipotunzwa na watumishi wenye mamlaka ya kutunza hizo nyaraka.

#### **Tulichojifunza**

#### **Taarifa nyingi kutoandaliwa kwa umakini**

Wakati wa uchambuzi wa taarifa za idara ya afya ilibainika kuwa taarifa nyingi haziandaliwi kwa umakini ambapo taarifa hizo hutofautiana au taarifa ambazo zimeandaliwa na idara hiyo.

#### **Ushiriki wa watumishi wa halmashauri**

Ushiriki wa watumishi wa halmashuri katika zoezi nzima la ufuutiliaji uwajibikaji jamii ni muhimu sana kwani husaidia kutoa ufanuzi kwa mambo ambayo yameibuka katika kipindi

cha uchambuzi wa taarifa hizo na pia huondoa mgogoro baina ya timu ya ufuatiliaji na halmashauri husika.

### **Utekelezaji wa miradi haufanyiki kwa ufanisi**

Kila mwaka kumekuwa na bakaa ya kiasi kikubwa cha fedha ambapo kimsingi inaathiri utoaji wa huduma ulio wenyе ufanisi na unaozingatia haki za msingi za binadamu. Kutokana na uchambuzi huu, tumejifunza kuwa shughuli nyingi ambazo zimeainishwa kufanyika katika CCHP hazikufanyika na matokeo yake kila mwaka kumekuwa na bakaa ya kiasi kikubwa cha fedha ambapo kimsingi inaathiri utoaji wa huduma ulio wenyе ufanisi na unaozingatia haki za msingi za binadamu.

### **Hitimisho na Mapendeleko**

Halmashauri kupitia baraza la madiwani inatakiwa kusimamia mfumo mzima wa uwajibikaji Jamii ili kuhakikisha kuna kuwa na uwazi na uwajibikaji kwa watumishi katika bajeti, hii itapelekea upatikanaji wa huduma iliyobora inayozingatia misingi ya kibinadamu.

Halmashauri katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi wa ufanisi ni lazima itumie taarifa za OPRAS katika kupata watumishi wenyе uadilifu wenyе kutimiza malengo yao na kusaidia kufikia malengo ya halmashauri, hii iligundulika wakati wa mahojiano na watumishi wa kada mbalimbali wakati wa kupata mtumishi aliyetukuta kwa mwaka huo wa fedha, iligundulika kuwa hakuna vigezo vyovytote vinavyowekwa na idara katika kumpata huyo mtumishi., hivyo ni vema halmashauri kuweka vigezo vitakavyoweza mpata mtumishi bora.

## **Marejeo**

1. Mpango mkakati wa halmashauri ya Ukerewe (SP-2008/2012),
2. Council's Comprehensive Health Plan (CCHP) 2010/2011,
3. Taarifa ya mwaka ya utekelezaji ya idara ya afya (2010/2012),
4. Taarifa ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali mwaka 2010/2011,
5. Taarifa ya mkaguzi wa ndani kuhusu mfuko wa jamii wa afya
6. Hoja za kamati ya fedha na mipango 2010/2011.